

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

MKUU WA MKOA WA NJOMBE

SIMU: 026- 2790001

FAX: 026- 2790001



OFISI YA MKUU WA WILAYA,

S.L.P 02,

LUDEWA.

**JULAI 04, 2022**

**TAARIFA KWA UMMA**

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mheshimiwa Andrea Tsere leo Julai 04, 2022 amemkaribisha Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ludewa.

Aidha Waziri wa Maliasili Mhe. Balozi Pindi Chana ameipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kwa kumuunga mkoni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuonesha wananchi wa Tarafa zote za Wilaya ya Ludewa filamu ya The Royal Tour na kuvumbua vivutio vya utalii vinavyo patikana Wilaya ya Ludewa ukiwemo Utalii wa utamaduni (ngoma za asili), Uwepo wa Ziwanyasa, utalii wa fukwe, utalii wa Misitua na safu za milima Livingstone nk.

Katika hatua nyingine Mhe. Waziri wa Maliasili na Utalii amekabidhi mizinga 300 ya kufugia nyuki katika vikundi mbalimbali vya Wilaya ya Ludewa wakiwemo Jumuiya ya watumiaji maji bonde dogo la mto Ketewaka.

**Chrispin B. Kalinga**  
**Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini**  
**Halmashauri (W) Ludewa**

